MAFUNZO YA WALIMU KAZINI NGAZI YA SHULE
KWA MWALIMU WA DARASA LA I-III

Moduli ya Kumi:

MISINGI YA KUANDIKA

Mwongozo wa Mratibu wa Mafunzo ya Walimu Kazini Ngazi ya Shule

UKaid
from the British people

equip Tanzania
Education Quality Improvement Programme

Moduli hii imetayarishwa kwa ushirikiano na:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Taasisi ya Elimu Tanzania
Chuo Kikuu cha Dodoma
Chuo cha Ualimu Morogoro
Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa
EQUIP-Tanzania

Moduli hii imewezeshwa kwa ushirikiano na:

C.C.U Butimba
C.C.U Bustani
C.C.U Tabora
C.C.U Ndala
C.C.U Kasulu
C.C.U Kabanga
C.C.U Bunda
C.C.U Tarime
C.C.U Shinyanga
C.C.U Mpwapwa

DIBAJI

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, imetoa kipaumbele katika sekta ya elimu ili kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii. Lengo la Dira ya Maendeleo ni kuwa na taifa la watu waliolelimika na jamii iliyo tayari kujifunza kufikia 2025. Serikali ya Tanzania imethibitisha kwa vitendo kuwa Elimu ni kiambato muhimu katika kupunguza umaskini na kuimarisha maendeleo ya taifa. Kwa muda mrefu serikali imetambua kuwa "Ubora wa Elimu yoyote hauwezi kuwa bora kuliko mwalimu mwenyewe" hivyo imetilia mkazo mafunzo kazini kwa walimu kupitia mikakati mbalimbali ili kuimarisha umahiri wa walimu katika ufundishaji na ujifunzaji darasani.

Katika kuongeza ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji darasani, Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kushirikiana na EQUIP-Tanzania, wameandaa moduli hii ambayo imesheheni kazi mbalimbali ambazo waalimu mtazitenda katika vikundi wakati wa mafunzo kwa kutumia mbinu ya Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule. Mbinu hii inatambua umuhimu wa walimu kujifunza pamoja na kubaini changamoto zinazowakabili ili kupata suluhisho la changamoto za ufundishaji na ujifunzaji kwa pamoja.

Moduli hii ya Mafunzo ya Walimu Kazini, imeandaliwa ili kusaidia juhudi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhakikisha kuwa mbinu fanisi zinatumika darasani wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Moduli hii pia inawasaidia walimu kushirikishana uzoefu na umahiri katika ufundishaji na ujifunzaji darasani. Vilevile Moduli inatoa mafunzo ya ziada ikitarajiwa kuwa walimu watakuwa wamekwisha pata Mafunzo Kabilishi ya utekelezaji wa Mtaala ulioboreshwa wa kuimarisha ufundishaji wa KKK kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili.

Taasisi ya Elimu Tanzania inatarajia kuwa moduli hii itawasaidia walimu kuimarisha umahiri wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuwasaidia wanafunzi waweze kujenga uwezo unaokusudiwa wakati wa kujifunza.

Changamoto iliyo mbele yetu ni kuhakikisha kuwa tunaonyesha kwa vitendo matokeo mazuri yanayotokana na maudhui ya moduli hii wakati wa ufundishaji na ujifunzaji darasani ili kuimarisha ubora wa elimu ya shule ya msingi.

Dr. Leonard Akwilapo
Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Taasisi ya Elimu Tanzania.

Maelezo Muhimu kwa Mratibu wa Mafunzo ya Walimu Kazini Ngazi ya Shule

Mwongozo huu utatumika sanjari na moduli ya kumi ya mwalimu ili kumsaidia mratibu wa mafunzo kuwa na mpangilio mzuri wenye kufuata hatua kwa hatua ili kuwafanya walimu washiriki kikamilifu katika kujifunza maudhui ya moduli ya kumi.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ambayo ni upande wa kushoto wa mwongozo unabeba maelezo ambayo mratibu wa mafunzo ya walimu kazini ngazi ya shule atatakiwa kuyafuata wakati wa kuratibu kipindi cha kujifunza maudhui ya moduli. Sehemu ya pili ambayo ni upande wa kulia wa mwongozo unabeba maudhui yaliyo kwenye moduli ya mwalimu ambayo watayasoma wakati wa kipindi cha kujifunza.

Wakati wa kipindi cha kujifunza, unatakiwa kufuata maelezo yanayokuongoza yaliyo upande wa kushoto wa mwongozo huu na kuyahusianisha na maudhui yaliyo kwenye moduli ya mwalimu ambayo yapo upande wa kulia wa mwongozo huu kama yanavyosomeka kwenye moduli ya mwalimu.

MAELEKEZO NA TASWIRA KATIKA MODULI

Kuna picha na michoro mingi katika moduli. Baadhi zinajirudia mara nyingi kwa sababu zinamaanisha jambo mahususi linalotokea. Zifuatazo ni mifano ya taswira mbalimbali ambazo zinapatikana katika moduli pamoja na kile ambacho zinawakilisha:

Jadili na mwenzako: Wakati wote wa kusoma moduli, walimu wataelezwa kufanya kazi pamoja na mwalimu mwingine juu ya maswali au kazi.

Fikiri– Wawili wawili – Shirikishana: Kama ilivyo katika maelezo ya hapo juu, hapa vilevile walimu wanafanya kazi wakiwa wawili wawili. Japokuwa, hapa walimu wanatafakari mmoja mmoja kwanza juu ya swali au tatizo, halafu mwalimu anafanya kazi na mwenzake na mwishoni wanawasilisha katika kundi lote.

Jadiliana katika kikundi: Wakati mwingine walimu wataelekezwa kutafakari au kujadili maswali mbalimbali katika kikundi.

Soma: Katika kila moduli kuna "dhana kuu" ambayo kwa kawaida huwasilishwa kwa kirefu katika maelezo.

Andika: Moduli itawahamasisha walimu kuchukua maelezo na kuandika fikra zao na majibu.

Igizo: Baadhi ya mazoezi yatahitaji walimu kuigiza kazi ya KUFUNDISHA wakati wengine watapaswa kuigiza kama wanafunzi.

MAELEKEZO KWA MRATIBU WA MAFUNZO YA WALIMU KAZINI

Kabla ya kuanza moduli hii, angalia 'maelekezo muhimu' na hakikisha kuwa wewe na walimu mnayatekeleza.

Tafadhali waambie walimu wajiorodheshe na kusaini hapa chini.

Tarehe:	Shule:	Wilaya:	Mkoa:
Muda wa kuanza:	Jina la Mratibu na sahihi yake:		
Muda wa kumaliza:	Jina la Mwalimu Mkuu na sahihi yake:		

	JINA LA MWALIMU	ME / KE	SAHIHI:	DARASA
1				
2				
3				
4				
5				
6				
7				
8				

WAAMBIE WALIMU:

"Sasa tutasoma utangulizi wa moduli hii. Tutasoma matini kwa sauti na kwa kupokezana. Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma aya ya kwanza, atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome aya inayofuata."

MODULI YA 10: MISINGI YA KUANDIKA

MAUDHUI YA MODULI

Moduli ya 5 – 8 inahusu dhana na mbinu za KUFUNDISHA kusoma ambazo zinaendana na mabadiliko yaliyo kwenye muhtasari mpya wa darasa la kwanza na la pili. Moduli hii pia inahusu baadhi ya dhana na shughuli kama zilivyoanishwa kwenye muhtasari mpya wa darasa la kwanza na la pili. Moduli hii inahusu misingi ya kuandika. Ujuzi wa kuandika siyo tu unawasaidia wanafunzi kuwasilisha mawazo na taarifa, pia kuwa na uwezo wa kuandika vizuri kunakoendana na uwezo wa mwanafunzi kusoma na kuelewa matini. Kwenye moduli hii, utajifunza mbinu za kuwafundisha wanafunzi namna ya kuandika, herufi za alfabeti, namna ya kutumia ujuzi wao wa foniki na herufi kuandika maneno. Somo la kuandika litaendelea kwenye moduli ya 13, ambapo utajifunza zaidi kuhusu kuandika na kusoma vinavyofanya kazi pamoja ili kumsaidia mwanafunzi aweze kusoma na kuandika.

DHANA KUU

1. **Kuandika herufi moja moja** – tumia mistari na vitanzi kutengeneza kila herufi moja moja ya alfabeti
2. **Kuandika maneno au 'Kuficha'**– Kinyume cha 'kuhusianisha' ambapo wanafunzi wanabainisha neno ambalo wanataka kuandika, wanaligawa kwenye sauti moja moja, na halafu wanaandika herufi inayoendana na kila sauti.
3. **Vitamkwa Vumbuliwa** – ni pale ambapo wanafunzi wanajaribu kuficha maandishi lakini wakapata kitamkwa kisicho sahihi kwa sababu baadhi ya maneno hayatamkwi kama inavyotakiwa. Hivyo wanafunzi wanapaswa wafanye mazoezi ya ujuzi wao wa foniki na watajifunza utamkaji sahihi baada ya kuona neno mara nyingi.
4. **Waandishi wanaotumia mkono wa kushoto** – wanafunzi ambao kwa asili wanaandikia mkono wa kushoto. Hawa hawapaswi kulazimishwa kuandikia mkono wa kulia kwa sababu uamuzi huo utaharibu uwezo wao wa kujifunza na kuwa makini.

MALENGO YA MODULI

Mwisho wa moduli hii, walimu watakuwa na uwezo wa:

1. Kuwajengea wanafunzi umahiri wa kuandika wakiwemo wanafunzi wanaoandikia mkono wa kushoto.
2. Kuelewa namna na kwa nini kuficha maandishi kupitia uandishi kunasaidia katika kusoma
3. Kutumia shughuli na mbinu za kuimarisha ujuzi wa mwanafunzi katika kuandika na kuficha maandishi
4. Tengeneza chati za mifukoni kusaidia mbinu za herufi/alama za uandishi

MAELEKEZO MUHIMU

Njoo na vitu vifuatavyo:

1. Moduli ya mafunzo ya walimu kazini na kalamu

TARATIBU ZA KUJIFUNZA KWA KILA KIPINDI

1. Kutana katika sehemu tulivu yenye ubao kama inavyoonekana katika picha
2. Panga madawati/meza ili kuwezesha washiriki wote waonane na kuongea kwa pamoja
3. Waeleze walimu wawe huru kuuliza maswali kama hawajaelewa
4. Waeleze walimu kuwa msaada kwa wenzao
5. Waeleze walimu kuwa wabunifu na kufikiria dhana watakazojifunza na jinsi zitavyohusiana na darasa lao
6. Waeleze walimu waweke simu zao katika hali ya mtetemo

TAFAKARI

WAAMBIE WALIMU:

“Tangu moduli ya 9, umefanyia mazoezi shughuli mbili kwenye kipindi cha kujifunza kusoma na kuandika. Orodhesha mafanikio uliyoyaona pamoja na changamoto ulizokabiliana nazo wakati wa KUFUNDISHA maudhui ya moduli hiyo darasani kwako. Una dakika 5 kwa ajili ya kazi hii.”

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutajadili kwa pamoja mafanikio na changamoto katika kikundi. Kwa kila changamoto ambayo imewasilishwa tufikiri kwa pamoja kuhusu namna ya kukabiliana nayo. Kumbuka kuandika ufumbuzi ambao unaweza kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Tutatumia dakika 10 kwa majadiliano.”

TAFAKARI

Katika kipindi cha mwisho tulisoma kuhusu kutenganisha na kuunganisha fonimu. Orodhesha mafanikio uliyoyaona pamoja na changamoto ulizokabiliana nazo wakati wa KUFUNDISHA maudhui ya moduli hiyo darasani kwako.

ANDIKA PEKE YAKO (DAKIKA 5)
Tafadhali andika kwenye visanduku mafanikio na changamoto ulizokutana nazo wakati wa kutekeleza mikakati hii katika darasa lako.

Mafanikio
(Elezea utaratibu uliotumia na fafanua jinsi ulivyofanikiwa)

Changamoto
(Elezea utaratibu uliotumia na fafanua changamoto zake)

JADILIANA KATIKA KIKUNDI (DAKIKA 10)

1. Shirikisha wenzako kwenye kundi mojawapo kuhusu uzoefu huo.
2. Kwa kila changamoto, pendekeza namna ya kukabiliana nayo.
3. Wakati wa majadiliano, andika ufumbuzi unaoendana na changamoto ulizobainisha.

Njia Muhimu za Ufumbuzi
(Mawazo muhimu na mahususi kwa wenzetu)

UTANGULIZI

WAAMBIE WALIMU:

“Leo tutaanza na baadhi ya shughuli za kuandika. Anza kwa kujaza herufi zinazokosekana kwenye chati ya kwanza. Baada ya kumaliza, jaza herufi zilizobakia kwenye chati ya pili, lakini mara hii, tafadhali tumia mkono wako mwingine kuandika. Kwa watu walio wengi, huu utakuwa mkono wao wa kushoto.”

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tumemaliza, tafadhali soma maswali kwa kujitegemea na fikiri kuhusu majibu yako. Jadili majibu yako na mwenzako. Kisha utashirikisha mawazo yako na kikundi.”

Jadili maswali yafuatayo hapa chini pamoja na mwenzako na kisha wasilisha majibu kwenye kundi zima:

1. Ni ujuzi gani umeufanyia mazoezi kwenye shughuli hizi?
2. Kulikuwa na changamoto zipi katika shughuli hizi?
3. Unadhani kulikuwa na kusudio gani katika shughuli ya pili?

(Wape walimu dakika 5 kujadili na kisha waeleze wajadili majibu yao. Kama walimu wamekwama, hapa kuna baadhi ya majibu)

1. Tulijifunza ujuzi wa kuandika
2. Ilikuwa ni changamoto kuandika kwa mkono wa kushoto
3. Lengo la kuandika kwa mkono ambao kwa kawaida huwa hauutumii ni kukuweka katika nafasi ya wanafunzi ambao wanajifunza kuandika kwa mara ya kwanza. Pia kukufanya ufahamu shida wanazopata wanafunzi wanaoandikia mikono ya kushoto, pale wanapolazimishwa kuandika kwa mikono ya kulia.

UTANGULIZI

ZOEZI LA KUCHANGAMSHA (DAKIKA 10)
Leo tutaanza na shughuli za kuandika. Anza kwa kujaza herufi zinazokosekana kwenye chati iliyoko hapa chini.

A a	___ b	Ch ___	D ___
___ e	___ ___	G ___	___ h
I ___	J ___	___ k	L ___

Sasa, jaza herufi za alfabeti zilizobakia, lakini safari hii, **tafadhali tumia mkono wako mwingine kuandika**. Kwa watu wengi, itawapasa kutumia mkono wao wa kushoto.

___ m	___ ___	O ___	___ p
R ___	S ___	___ ___	U ___
___ v	W ___	Y ___	___ z

FIKIRI – JOZISHA – SHIRIKISHANA (DAKIKA 5)

Jadili maswali yafuatayo hapa chini pamoja na mwenzako na kisha wasilisha majibu kwenye kundi zima:

1. Ni ujuzi gani umeufanyia mazoezi kwenye shughuli hizi?
2. Kulikuwa na changamoto zipi katika shughuli hizi?
3. Unadhani kulikuwa na kusudio gani katika shughuli ya pili?

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutasoma maudhui muhimu. Tutasoma kwa sauti matini kwa kupokezana.

Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma aya ya kwanza, atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome aya inayofuata.

Wakati wa kusoma weka alama zifuatazo kwenye matini unayosoma.

Weka alama ya mshangao (!) Kwenye wazo ambalo unadhani ni muhimu.

Weka alama ya kuuliza (?) Kuonesha kutokukubaliana na dhana hiyo au huelewi.

Weka alama ya mduara (O) kuonesha kuwa dhana hiyo ni mpya kwako.”

DHANA KUU

MISINGI YA KUANDIKA (DAKIKA 25)

1. Mwalimu mmoja aanze kusoma kwa sauti. Baada ya kukamilisha sehemu (kwa mfano, aya au maelezo) amwite mwalimu mwingine kwa jina asome sehemu inayofuata.
2. Wakati unaposoma zingatia alama zifuatazo:
    - Weka alama ya mshangao (!) katika sehemu ambayo unaona ni muhimu.
    - Weka alama ya kuuliza (?) katika sehemu ambayo huelewi au hukubaliani nayo.
    - Weka mduara katika (o) maneno ambayo ni mapya.

Kuandika ni uwezo kuweka mawazo au dhana katika maandishi kwa ajili ya kusoma. Hata hivyo, kabla wanafunzi hawajafikisha mawazo na taarifa kupitia kuandika, lazima wafahamu namna ya kuumbaandika herufi kwenye kurasa.

Kuandika herufi moja moja

Ili kuwasiliana kupitia matini, wanafunzi lazima wawe na uwezo wa kuumba herufi ambazo zinaundwa kwa usahihi, uthabiti na kwa uwazi. Kujifunza kuandika herufi moja moja lazima kuanze kwenye mizania kubwa na polepole ikijielekeza mahali kunakolengwa. Kwa mfano, wafundishe wanafunzi wako kufanya mambo yafuatayo:

1. Kwanza kuandika herufi moja moja kwa kutumia vidole vyao hewani
2. Halafu kuandika herufi moja moja kwa kutumia vidole vyao kwenye dawati, ardhini, au kwenye mchanga
3. Tena, kuandika herufi kwa kutumia penseli kwenye karatasi yoyote
4. Mwisho, kuandika herufi kwa kutumia penseli kwenye mistari (mistari miwili miwili kama ipo)

KUFUNDISHA kuandika kwa njia hii kunaruhusu wanafunzi kukuza uwezo wao wa kudhibiti mikono yao na vidole.

Wanafunzi pia watajifunza kuumba herufi kwa kukuangalia ukiandika ubaoni. Wakati unaandika neno kwenye ubao, fanya uwezavyo kuandika kwa unadhifu katika ukubwa ambao wanafunzi wanaweza kuona vizuri (kwa kukadiria ukubwa wa mkono wako). Mara zote chapisha maneno – usiyaandike kwa kuyaviringisha. Hapa chini kuna mfano unaoweza kuufuata (siyo muhimu kwa walimu wa Darasa la 1 KUFUNDISHA herufi kubwa na ndogo kwa wakati mmoja).

Kumbuka, unaweza kuanza na herufi zinazofahamika sana: irabu a, e, i, o, u na kisha konsonati b, m, k, d, n. Hata hivyo, kuwa makini na baadhi ya herufi ambazo zinachanganywa kirahisi na wengine kwa sababu zinakaribia kufanana kwa maumbo, kama vile m-n, b-d, n-u na a-o. Jaribu kutofundisha herufi hizi kwa pamoja na ruhusu muda wa kutosha kwa wanafunzi kujifunza herufi moja kabla ya kuwaanzishia herufi nyingine.

Konsonati zinazofuata na ambazo hazifahamiki sana ni: l, t, p, s, f, j. Kundi la mwisho la herufi ni: g, y, z, h, r, w, v, ch. Kuwa makini na w-v kwa sababu zinafanana na zinaweza kuwachanganya wanafunzi.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

DHANA KUU

Mchakato huu unafanana sana kwa wanafunzi ambao wanajifunza kusoma:



Kama ilivyojadliwa kwenye moduli ya 8, chagua herufi ya kujielekeza kwa ajili ya somo. Baada ya kutumia mbinu ya **Jina-Neno Kuu-Sauti KUFUNDISHA jina la herufi na sauti,** unaweza tena kuwaonesha wanafunzi namna ya kuandika neno kwanza hewani, halafu kwenye dawati, halafu kwa penseli au katika karatasi isiyo na mistari, na mwisho kwenye karatasi yenye mistari

Wanafunzi wanaoandikia Mkono wa Kushoto

Kwa kukadiria, asilimia 25 ya watu walioko duniani kwa asili wanaandika kwa kutumia mkono wa kushoto. Wanasayansi wengi wanaamini kuwa uwezo wa mtu kuandikia mkono wa kulia au wa kushoto unabainishwa kabla hajazaliwa. Inapaswa kueleweka kuwa utumiaji wa mkono wa kushoto siyo upungufu – wanafunzi ambao huandikia mkono wa kushoto wanaweza kufanya shughuli zilezile ambazo watoto wanaoandikia mkono wa kulia wanaweza kuzifanya, hatahivyo katika muktadha mbalimbali, kuandika kwa kutumia mkono wa kushoto hakushauriwi sana.

Kumlazimisha mwanafunzi ambaye kwa asili anaandikia mkono wa kushoto, aanze kutumia mkono wa kulia, siyo tu ni kinyume cha asili na kumkosesha utulivu mwanafunzi, bali linaweza kuwa na athari mbaya kwenye kujifunza kwake. Mwanafunzi atatumia nguvu kubwa ya akili kujaribu kudhibiti mkono wake anaouandikia kwa kulazimishwa kuliko kutumia akili hiyo kujifunza ujuzi wa awali wa kuandika (hii inaweza kuwa namna ulivyojisikia wakati wa zoezi la kuchangamsha).

DHANA KUU

Sema neno la kwanza kisha wape walimu muda wa kuandika neno hilo kwa kificho. Mara wakishamaliza, sema neno la pili na waruhusu waandike. Halafu sema neno la mwisho:

1. fua
2. sita
3. mkate

Mara walimu wote wanapomaliza, waeleze waoneshe majibu yao kwenye kundi



DHANA KUU

Kama walimu, lazima tutambue na kuwakubali wanafunzi wetu wanaotumia mkono wa kushoto kwa asili (na kuwaeleza wazazi wao kuwa hali hiyo ni ya asili). Kuna mbinu nyingine ambazo tunaweza kuzitumia kuwasaidia wanafunzi wa aina hii:

Namna ya kuwasaidia wanafunzi wanaoandikia kwa mikono ya kushoto:

1. Waeleze wanafunzi wakae upande wa kushoto wa madawati yao ili wasiwagonge wenzao kwa mikono
2. Wakalishe wanafunzi upande wa kushoto wa darasa ili wewe unapokuwa ubaoni wasilazimike kukuangalia kupitia mikono yao ya kushoto ambayo wanaiandikia.
3. Zungusha madaftari yao au karatasi za kuandikia ili sehemu ya juu kushoto iwe juu zaidi ya sehemu ya juu kulia. Hii inawasaidia wanafunzi kuona vizuri kile wanachoandika.
4. Hamasisha wanafunzi wanaoandikia mikono ya kushoto waweke mikono na vifundo vya mikono yao moja kwa moja na chini ya mstari wa kuandikia. Wanafunzi wengi wana tabia ya kugeuza vifundo vyao ili waandike kutokea juu ya mstari. Hatahivyo, hii inawafanya waandike kwa shida na inaweza kusababisha matatizo na vifundo vyao. Kuzungusha dafatari kunasaidia jambo hili.

Kuandika Maneno

Mara wanafunzi wanapokuwa na uwezo wa kuandika herufi moja moja, watatumia ujuzi wa foniki kuandika maneno. Sasa tufanye shughuli ifuatayo kuonesha. Kwanza, Mratibu wa Mafunzo Kazini atasema neno kwa sauti. Halafu tumia alama katika jedwali ufuatao kuandika neno kwa siri.
Usitumie herufi za alfabeti isipokuwa kuandika irabu A au I.



1. _____

2. _____

3. _____

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Vema, tuendelee na zoezi la kugeuka na kusoma”

WAAMBIE WALIMU:

“Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

DHANA KUU

Kuandika maneno kwa kutumia sauti za herufi

Kama ulivyopata uzoefu, kuandika maneno kwenye karatasi kunajumuisha kutambua neno ambalo unataka kuandika, kutenganisha sauti za herufi katika neno, halafu kuandika herufi zinazoendana na sauti hizo. **Mchakato huu wa kuandika maneno unaitwa "Kuficha Maandishi", ambao unatumia ujuzi wa wanafunzi wa 'kuhusianisha', lakini kwa kinyume.**

Kuhusianisha (kama tulivyojifunza kwenye Moduli ya 9)

Andika maneno kupitia sauti za herufi (Kuficha)

Kuangalia uandishi kwa namna hii, tunaweza kuona kwamba kuandika na kusoma ni njia zinazotumia ujuzi wa foniki wa wanafunzi. Mara tu wanafunzi wanapokuwa na weledi na kila sauti ya herufi ya alfabeti, pamoja na namna ya kuandika kila herufi. Watakuwa na uwezo wa kuandika neno kwenye karatasi. Unapaswa kuwapa wanafunzi fursa nyingi kufanya mazoezi ya kuficha maneno kwa kutumia mbinu ya 'Ninafanya – Tunafanya- Unafanya'. Kwa mfano:

1. Chukua neno linalotumia sauti za herufi ambazo wanafunzi wanazifahamu vizuri kama vile 'paka'. Tamka neno kwa sauti.
2. Anza na 'Ninafanya': Waoneshe wanafunzi kwamba wanaweza kutumia mbinu kama Binya Vidole kutenganisha sauti za herufi katika neno.
3. Kwa kila sauti herufi iliyotambuliwa, waulize wanafunzi wakwambie ni herufi zipi zinakwenda na kila sauti
4. Mwanafunzi anapotambua herufi kwa usahihi, mweleze aje mbele ya darasa na umpe kadi ya herufi ashikilie ili kila mmoja aione. (Kama hauna kadi ya herufi, unaweza kuandika herufi kwenye ubao wakati wanafunzi wanazitambua)
5. Fanya hivi kwa kila herufi ili kuwe na kundi la wanafunzi lililosimama mbele ya darasa, likishikilia kila herufi ambayo inaunda neno 'paka'
6. Endelea na 'Tunafanya': Waeleze wanafunzi wafanye zoezi la Binya Vidole pamoja na wewe. Mueleze kila mmoja aseme herufi inayoendana kwa kila sauti na waombe wanaojitolea washikilie kadi herufi. Ukishakuwa na wanafunzi walioshikilia kadi herufi, elekeza darasa zima liandike kila herufi kuunda neno (kwenye madaftari yao)
7. Malizia na 'Unafanya': Sema neno "paka" na waeleze wanafunzi kwa kujitegemea kila mmoja wao, watenganishe sauti herufi, watambue herufi zinazoendana na sauti, na kisha waandike maneno kwenye madaftari yao.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa kila mwalimu anaweza kushirikisha jambo aliloona ni muhimu, halieleweki au ni jipya. Kisha tunaweza kujadili kuhusu namna gani ujuzi wa kuhusianisha unajenga uwezo wa wanafunzi kuandika.”

Eleza kila mwalimu atoe majibu yake. Kama walimu wanakwama juu ya swali la 4, hapa kuna jibu ambalo unaweza kuwashirikisha:

Jibu la 4: Mchakato wa kuandika kwa kutumia ujuzi wa wanafunzi wa kuhusianisha lakini kwa kinyume. Kuandika maneno kunajumuisha kutambua neno ambalo unataka kuandika, kutenga sauti katika neno, kisha andika herufi zinazoendana na sauti hizo.

DHANA KUU

Andika maneno kwa kutumia silabi

Wanafunzi wanaweza pia kuvunjavunja maneno kuwa silabi wanazozijua, na kisha wakaandika kila silabi kuunda neno lililoandikwa:

Kuandika neno kutokanana na sauti ya silabi

Wakati mwingine, wanafunzi wangependa kuandika neno ambalo linajumuisha silabi zinazoungwa kwa herufi mwambatano na irabu. Hii inapotokea, wanafunzi wanaweza kutenganisha silabi zinazoungwa herufi mwambatano na kuwa sauti/herufi moja moja.

Kuandika neno kupitia matumizi ya sauti za herufi na silabi

Fanya mazoezi ya kuandika maneno

Wakati wanafunzi wanaandika, ni muhimu uwashauri waandike herufi zinazoendana na sauti au silabi wanazosikia. Hatahivyo, wakati mwingine wanafunzi wanaandika neno likiwa na matamshi yaliyokosewa kwa sababu baadhi ya maneno hayatamkwi kama yanavyosemwa. Hii ni sawa! Hii inaitwa vitamkwa vumbuliwa. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kuandika neno "ng'ombe" kama hivi: gombe. Hii ni kwa sababu mwanafunzi bado hajajifunza sauti ya "ng" (hii inaweza kutokea pamoja na herufi mwambatano zingine) kama "dh", "ny" na "gh".

Badala ya kusahihisha utamkaji wa wanafunzi hapo hapo, waruhusu watumie ujuzi wao wa foniki kutamka maneno kama wanavyoyasikia. Kadri muda utakavyokuwa unakwenda, kupitia mazoezi endelevu ya kusoma na maelekezo ya msamiati, wanafunzi watajifunza na kukumbuka matamshi sahihi.

MAJADILIANO KATIKA KIKUNDI (DAKIKA 10)

1. Maudhui gani umewekea alama ya mshangao (!)?
2. Maudhui gani umewekea alama ya kuuliza (?)?
3. Maudhui gani umezungushia alama ya mduara?
4. Ni namna gani ujuzi wa kuhusianisha unajenga uwezo wa wanafunzi kuandika?

ZOEZI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa, tutafanya zoezi la mbinu ya KUFUNDISHA wanafunzi uundaji wa herufi. Mbinu hii inaweza kutumika wakati wowote ambapo wanafunzi wanajifunza herufi na sauti zao. Baada ya mwalimu wa kwanza kumaliza sehemu au maelekezo, anaweza kuita jina la mwalimu mwingine ili asome zinazofuatia.

Angalizo: Tunapoandika hewani kwa kutumia mkono tunatumia kidole kimoja na sio viwili kama ilivyoelezwa na kuoneshwa kwenye picha.”

Wakati washiriki wanasoma maelekezo, andika herufi “n” kwa ukubwa sana (ifikie nusu mita kwa urefu) kwenye ubao.



ZOEZI

IGIZO (DAKIKA 20)

wakatı unapotambulisha herufi mpya kuna njia nyingi za KUFUNDISHA uundaji herufi sahihi. Shughuli hii hapa chini inakupitisha kwenye uandikaji wa hewani, kuandika kwenye dawati na halafu kuandika kwenye karatasi. Kwa kutumia mbinu hizi, wanafunzi wanatumia misuli yote ya mabega na mikono. Hii inaifanya misuli iendane na uumbaji wa kila herufi na kusaidia kuhakikisha kwamba, pamoja na mazoezi endelevu, mwanafunzi anaandika herufi kwa usahihi zaidi kila wakati. Mratibu wa Mafunzo Kazini atafanya Igizo hili wakati mwalimu na kila mtu aliyebakia wakijifanya kuwa wanafunzi.

1. Mratibu wako wa Mafunzo Kazini ataandika herufi kubwa kwenye ubao

2. Simama na shikilia kidole kimoja kwa kutumia mkono wako wa kulia. Kidole hiki kitakuwa kama 'penseli' yako wakati unaandika hewani.

3. Nyoosha mkono wako na onesha "kidole penseli" chako kuelekea mahali ambapo herufi inaanzia kwenye ubao. Mratibu wa Mafunzo Kazini atakwambia kutafuta herufi kama vile ulikuwa unaandika herufi hewani kwa kutumia "kidole penseli" vyako. Hakikisha unaweka kidole chako na mkono kwa uimara. Tembeza mkono wako wote kutoka begani kwako, siyo kiwiko chako au kifundo.



4. Nyoosha mkono wako, na rudia kuandika 'n' hewani. Halafu, fanya hatua zile zile ukiwa umefumba macho yako.

ZOEZI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tafadhali chukua penseli yako na fanya zoezi la hatua nne kuonesha wanafunzi namna ya kushikilia penseli kwa usahihi. (Waangalie washiriki wakati wanajaribu hatua hizi.) “

ZOEZI

5. Rudia hatua ya 2 – 4 kwa mkono wako wa kushoto. Hii ni njia moja ya kuwasaidia wanafunzi kubaini kama wanajiona wako katika hali nzuri kuandika kwa kutumia mikono yao ya kushoto. Kama wanafunzi wakiona kuandika hewani ni rahisi kwa kutumia mkono wa kushoto, washauri wajaribu kutumia mikono yao ya kushoto kuandika.

6. Baada ya kuandika 'n' hewani, tumia kidole cha shahada na cha kati "kidole penseli" kuandika herufi ile ile kwenye dawati. Mara hii unaweza kupindisha mkono wako ili uwe kama unaadika. Andika herufi kubwa 'N' kwenye dawati lako. Fanya hivi tena ukiwa umefumba macho yako. Kama wanafunzi wakiona ni rahisi kutumia njia hii kwa mikono yao ya kushoto, wanapaswa kutumia mikono ya kushoto kuandika.

Baada ya kuandika herufi kwenye dawati lako, jiandae kuandika herufi kwa kutumia kalamu yako. Kama wanafunzi wako bado hawajui kushikilia penseli sawasawa, tumia mbinu ya 'kibanio na kishtuzi' kuweka mikono yao kwenye sehemu sahihi kama inavyoonyeshwa kwenye picha hapa chini.

HATUA YA 1:
Shikilia kalamu ili ncha iwe katikati ya kidole gumba na kidole cha shahada.

HATUA YA 2:
Tumia mkono wako wa pili kuzungusha kalamu ili ncha iangalie chini.



HATUA YA 3:
Endelea kuzungusha kalamu hadi itulie kwenye mkono wako na ncha ikiangalia mbali na wewe.



HATUA YA 4: Leta mbele vidole vyako vitatu vilivyobakia ili kalamu ikae kwenye kidole chako cha katikati.

KUPANGA MKAKATI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tumemaliza zoezi la kuandika angani, tujibu maswali yafuatayo katika kundi.”

1. Ni namna gani hivi sasa unawafundisha wanafunzi kushikilia kalamu zao na kuumba herufi?
2. Ni namna gani kuandika hewani na kwenye dawati kunasaidia ujuzi wa wanafunzi katika uandishi?
3. Ni hatua gani nyingine ambazo unaweza kutumia mbinu hizi katika mazingira ya darasani kwako?
4. Ni namna gani utaweza kutumia mbinu hii kwenye masomo yako?

Mwelekeze mwalimu anayejitolea kusoma maswali ya mjadala kwa sauti.
Wape washiriki 2 – 3 fursa ya kujibu baada ya kila mmoja.

1: wanafunzi wanafanya mazoezi ya kuandika herufi na maneno mafupi katika sehemu kubwa kwa mara ya kwanza, kisha wanaanza kuandika kwa udogo zaidi ili kukuza uimara wa misuli.

2: wanafunzi wanaweza kuandika juu ya meza au chini, wanaweza kuandika huku vidole vyao vikiwa nyuma ya kila mmoja wao au viganja

3: wanafunzi wanaweza kufanya zoezi la kuandika herufi angani wakati wanajifunza sauti au maneno mapya

KUPANGA MKAKATI

7. Baada ya kuwaonesha wanafunzi mbinu ya'kibanio na kishtuzi', tembea kuzunguka darasa kuhakikisha kuwa kila mmoja anafanya kwa usahihi. Halafu tumia mikupuo uliyotumia pamoja na 'vidole kalamu' vyako kuandika herufi 'n' kwa kutumia kalamu yako. Andika herufi kubwa kwenye karatasi isiyo na mistari. Kama huna karatasi isiyo na mistari, chora herufi kubwa 'n' kwenye karatasi ilinyooshwa halafu chora herufi kwa muendelezo huo huo lakini ikiwa ndogo.

Mbinu kama hizi zinasaidia wanafunzi wanaotumia mikono ya kushoto na mikono ya kulia kuandika kwa sababu wanaanza na eneo kubwa (hewani) na wanaendelea kuandika kuja kwenye eneo dogo (dawati) hadi kwenye sehemu yote ya karatasi, kwenye mistari ya karatasi). Taratibu huu unaifanya misuli kwenye mikono izoee na hivyo kuwezesha wanafunzi waweze kuandika kwenye karatasi kwa usahihi tena kwa ukubwa unaohitajika.

Kuandika hewani kunaweza kutumika kufanyia mazoezi mbinu nyingine pia!

Kufanya mazoezi ya Foniki:
Kufanya mazoezi ya maneno yaliyounganishwa kwenye sauti za herufi, taja sauti za herufi (usiiandike kwenye ubao) na waulize wanafunzi 'kuandika' hewani herufi ambayo imetokana na sauti hiyo.

Kuandika Silabi, maneno yanayoonekana na maneno msamiati:
Badala ya kuandika herufi moja tu kwenye ubao, andika silabi, maneno yanayoonekana, au maneno ya msamiati ambayo wanafunzi wanajifunza. Waeleze wanafunzi "waandike" hewani neno lililoko ubaoni.

JADILI PAMOJA NA KIKUNDI (DAKIKA 5)

Baada ya kufanyia mazoezi shughuli hii, jadili swali pamoja na kundi:

1. Ni namna gani hivi sasa unawafundisha wanafunzi kushikilia kalamu zao na kuumba herufi?
2. Ni namna gani kuandika hewani na kwenye dawati kunasaidia ujuzi wa wanafunzi katika uandishi?
3. Ni hatua gani nyingine ambazo unaweza kutumia mbinu hizi katika mazingira ya darasani kwako?
4. Ni namna gani utaweza kutumia mbinu hii kwenye masomo yako?

KUPANGA MKAKATI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutapanga vipindi vyetu vya kusoma na kuandika. Tutasoma maelekezo kwa pamoja na kwa sauti. Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma sehemu, anaweza kuita jina la mwalimu mwingine kusoma sehemu inayofuatia.”

KUPANGA MKAKATI

KUAANDAA KIPINDI CHA "KUSOMA NA KUANDIKA" (DAKIKA 25)

Ili kukuza uwezo wa wanafunzi kusoma, ni muhimu sana kwamba aweze kufanya mazoezi juu ya mbinu mpya za kusoma na kuandika alizosoma kutoka kwenye Mafunzo ya Walimu Kazini. Kurasa zifuatazo zinajumuisha masomo ya jumla yanayoelekeza shughuli ambazo unaweza kujaribu wakati wa kipindi chako cha kusoma na kuandika (au unaweza pia kujaribu wakati wa kipindi chako cha kawaida cha Kiswahili). Pamoja na mwenzako:

1. Soma kwenye mpango wa masomo.
2. Jaza nafasi zilizo wazi mahali panapohitaji hivyo.
3. Jaribu masomo wakati wa kipindi cha kusoma na kuandika.

Angalia maelezo yaliyotolewa katika moduli ya 9 kuhusu mwongozo wa somo.

MWONGOZO WA MASOMO 1: Andika herufi za alfabeti HATUA ZA KUFUNDISHA	
HATUA	**SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA**
UTANGULIZI	1. Waambie wanafunzi kwamba watafanya mazoezi ya kuandika herufi 'm'. Unaweza kutumia mbinu ya 'Ninafanya – Tunafanya – Mnafanya', kuonesha namna ya kuandika herufi. 2. Anza na 'Ninafanya': Simama na shikilia vidole viwili kwa kutumia mkono wako wa kulia. Vidole hivi vitakuwa kama 'penseli' yako ukiwa unaandika hewani. 3. Nyoosha mkono wako na geuka ili uelekeze "vidole penseli" vyako kuelekea mahali ambapo herufi zinaanzia kwenye ubao. Hakikisha wanafunzi wanaona na kuelewa kile unachofanya. 4. Tafuta herufi kama vile ulikuwa unaandika herufi hewani kwa kutumia "vidole penseli" vyako. Hakikisha vidole na mkono wako vinakuwa imara, tembeza mkono wako wote kutoka begani kwako, siyo kiwiko chako au kifundo. 5. Endelea na 'Tunafanya': Waeleze wanafunzi wasimame, watumie kidole kama 'penseli' yao, elekeza penseli yao kwenye herufi iliyoko ubaoni na waandike herufi hewani. Fanya hivi pamoja nao ili waweze kufuata vitendo vyako. 6. Malizia na 'Mnafanya': Waeleze wanafunzi waandike herufi hewani kwa kujitegemea. Zunguka darasani na hakikisha wanafunzi wanaandika herufi kwa usahihi. 7. Rudia kwa kutumia mkono wa kushoto. Hii ni njia ya kusaidia wanafunzi kutambua ikiwa wanakuwa huru zaidi kuandika kwa kutumia mkono wa kushoto.
MAPYA	1. Baada ya kuandika herufi ya siku hewani, waeleze wanafunzi wakae chini na watumie vidole vyao vya shahada na vya kati 'vidole penseli' kuandika herufi ile ile kwenye madawati yao. 2. Waambie kwamba wanaweza kupindisha mikono yao kuonesha kama vile wanaandika. Waambie watumie 'vidole penseli' vyao kuandika toleo kubwa la herufi ya siku kwenye madawati yao mara nyingi 3. Unaweza pia kuwaeleza wanafunzi wakae wawiliwawili na waeleze waandike herufi katika mgongo wa kila mmoja. Tena, tembea darasani kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaandika herufi kwa usahihi.

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
IMARISHA	1. Ikiwa wanafunzi wako ndiyo wanajifunza kutumia penseli, tumia mbinu ya 'Ninafanya – Tunafanya – Mnafanya' kuonesha namna ya kushikilia penseli. 2. Anza na ' Ninafanya': Shikilia penseli na kuhakikisha kuwa ncha iko kati ya dole gumba na kidole cha shahada (angalia picha kwenye sehemu ya shughuli katika moduli hii). 3. Tumia mkono wako mwingine kuzungusha penseli ili ncha iangalie chini 4. Endelea kuzungusha penseli hadi ikae mkononi mwako na ncha ikiangalia mbali na wewe 5. Leta mbele vidole vyako vitatu vilivyobakia ili penseli ikae kwenye kidole chako cha katikati 6. Endelea na 'Tunafanya': Rudia hatua ya 2 – 5 wakati ukifanya pamoja na wanafunzi 7. Malizia na 'Mnafanya': Waambie wanafunzi warudie hatua ya 2 – 5 peke yao. Tembea kuzunguka darasani na saidia wanafunzi wenye matatizo. 8. Mara tu kila mmoja akishikilia penseli kwa usahihi, waeleze wanafunzi watumie mikupuo waliyotumia kwenye "vidole penseli" vyao kuandika herufi ya siku pamoja na penseli yao.
FANYIA MAZOEZI	9. Kama una nmuida wa ziada fanya mazoezi ya kutosha kwa herufi zingine
KUPIMA	1. Kwa herufi ambazo umekwishazifundisha, sema jina la herufi au sauti (usiandike herufi hizi ubaoni) na waelekeze wanafunzi waandike herufi hewani kwa kutumia vidole vyao. 2. Kisha waambie waandike herufi kwenye madawati yao na kwenye karatasi. 3. Tembea kuzunguka darasani na rekodi kwenye kumbukumbu zako ikiwa wanafunzi wanaandika herufi kwa usahihi. 4. Weka rekodi ya herufi zinazotatiza na rudia KUFUNDISHA namna ya kuandika herufi hizi katika kundi dogo. Unaweza pia kuwaweka wanafunzi wawiliwawili katika makundi yenye wanafunzi werevu ambao wanaweza kuwasaidia hawa wenye matatizo

Tathmini: _____

Maoni: _____

Angalia maelezo yaliyotolewa katika moduli ya 9 kuhusu mwongozo wa somo

MWONGOZO WA SOMO LA PILI: Andika herufi kupitia Kuficha Maandishi

HATUA ZA KUFUNDISHA

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
MAANDALIZI	1. Kabla ya somo, andaa orodha ya maneno ambayo wanafunzi wanajifunza au tumia orodha hii hapa chini ambayo imechukuliwa kutoka kwenye mtaala wa Kiswahili kwa kila darasa. 2. Kuwa huru kuja na orodha yako mwenyewe na hakikisha unatumia maneno ambayo yana sauti za herufi na silabi ambazo wanafunzi wanazifahamu. 3. Chagua walau maneno 2 – 3 ambayo yana silabi ambazo wanafunzi wako wanaweza kuwa hawazifahamu. Kwa mfano, 'shamba', 'mwalimu' na 'nyumbani'.

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

<table>
<tr><th>HATUA</th><th>SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA</th></tr>
<tr><td>MAANDALIZI</td><td>
<table>
<tr><th>Maneno kwa ajili ya darasa la 1</th><th>Maneno kwa ajili ya darasa la 2</th><th>Maneno kwa ajili yadarasa la 3</th></tr>
<tr><td>Mama
Baba
Mimi
Jina
Kitabu
Kalamu
Meza
Vikombe
Shamba</td><td>Kofia
Koti
Viatu
Vijiko
Wanyama
Wadudu
Baridi
Mrefu
Mwalimu</td><td>Sokoni
Singizia
Jenga
Katili
Ulimbo
Huruma
Kalenda
Mizani
Nyumbani</td></tr>
</table>
</td></tr>
<tr><td>UTANGULIZI</td><td>1. Waambie wanafunzi kwamba wanakwenda kufanya mazoezi ya kaundika maneno kulingana na sauti zao za herufi.
2. Chagua neno kutoka kwenye orodha yako ya maneno na litamke kwa sauti. Halafu tumia mbinu ya ‘ Ninafanya – Tunafanya – Mnafanya’ kuwasaidia wanafunzi wafanye mazoezi ya kuficha neno.</td></tr>
<tr><td>KUJENGA UMAHIRI</td><td>1. Chagua neno kutoka kwenye orodha yako ambalo linatumia sauti za herufi ambazo wanafunzi wanazifahamu vizuri, kama “jina”. Sema neno kwa sauti. Anza na ‘Ninafanya’: Onesha wanafunzi kwamba wanaweza kutumia mbinu ya Binya Vidole kutenganisha sauti za herufi katika neno. Kwa kila sauti ya herufi ambayo imetambuliwa, waambie wanafunzi wakwambie herufi gani inakwenda na kila sauti. Mwanafunzi akitambua herufi kwa usahihi, muombe aje mbele ya darasa na mpe kadi ya herufi ya kushikilia ili kila mtu aione. (Kama hauna kadi ya herufi, unaweza kuandika herufi kwenye ubao wakati wanafunzi wakizitambua). Fanya hivi kwa kila herufi ili kuwe na kundi la wanafunzi waliosimama mbele ya darasa, wameshikilia kila herufi ambayo inaunda neno “jina”. Endelea na ‘Tunafanya’: Waambie wanafunzi wafanye zoezi la Binya Vidole pamoja na wewe. Elekeza kila mmoja aseme herufi ambayo inaendana na kila sauti na omba anayejitolea ashikilie kadi ya herufi. Ukishakuwa na wanafunzi walioshikilia kadi za herufi, waambie wanafunzi wote darasani waandike kila herufi inayounda neno (kwenye madaftari yao)
2. Malizia na ‘Mnafanya’: sema neno “jina” na waambie wanafunzi kila mmoja akiwa peke yake atenganishe sauti za herufi, atambue herufi ambazo zinaambatana na sauti, na kisha aandike maneno kwenye daftari lake.</td></tr>
<tr><td>IMARISHA</td><td>1. Chagua neno kutoka kwenye orodha yako ya maneno na litamke kwa sauti, kama “kitabu”.
2. Anza na ‘Ninafanya’: Waoneshe wanafunzi kwamba wanaweza kutumia mbinu kama vile Kupiga Makofi kwa silabi (kutoka moduli ya 7) hadi kutenganisha silabi katika neno
3. Waoneshe namna ‘kupiga makofi’ katika silabi za neno kunafanya usikie kila silabi peke yake
4. Waulize wanafunzi herufi zipi zinatengeneza silabi. Mwanafunzi anapojibu kwa usahihi (“ki”), mwambie aje mbele ya darasa na mpe kadi za herufi ashikilie na kila mmoja aone. (Kama huna kadi za herufi, unaweza kuandika herufi ubaoni wakati wanafunzi wanazitambua).
5. Fanya hivi kwa kila silabi hadi kuwe na wanafunzi watatu wamesimama mbele ya darasa, wakishikilia silabi: “ki” “ta” “bu”
6. Endelea na ‘Tunafanya’: Watake wanafunzi wapige makofi kwa silabi pamoja na wewe. Elekeza kila mmoja aseme herufi inayoendana na kila silabi na uliza wanaojitolea kushikilia kadi herufi. Mtake kila mwanafunzi aandike kila silabi kuunda neno (kwenye madaftari yao). Malizia na ‘Mnafanya’: sema neno “kitabu” na waeleze wanafunzi kila mmoja na kwa kujitegemea watenganishe silabi, watambue herufi ambazo zinaendana na silabi, na kisha waandike maneno kwenye madaftari yao.</td></tr>
</table>

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
KUTUMIA UMAHIRI	1. Waambie wanafunzi kwamba wanakwenda kufanya zoezi la kuandika maneno kutokana na sauti za herufi pamoja na silabi zao. 2. Chagua neno kutoka kwenye orodha yako ya maneno ambayo ina silabi ambazo wanafunzi wanaweza kuwa hawazifahamu. Kwa mfano 'mwalimu'.. 3. Anza na 'Ninafanya': Onesha wanafunzi kwamba wanaweza kutumia mbinu kama Kupiga Makofi kwa Silabi ili kutenganisha silani katika neno: /mwa/ /li/ /mu/ 4. Mara tu ukishapiga makofi kwa silabi zote, tumia Binya Vidole kutenganisha sauti za herufi katika silabi hiyo. 5. Gusa kila sauti herufi na waambie wanafunzi watambue herufi zinazoenda na kila sauti ya herufi: /m/ /w/ /a/ 6. Mwanafunzi anapojibu kwa uhakika, mwambie aje mbele ya darasa na mpe kadi herufi kushikilia kiasi cha kila mmoja kuiona. 7. Fanya hivi kwa kila sauti herufi na silabi ili kuwe na wanafunzi 6 waliosimama mbele ya darasa: watatu wakiwa wameshikilia herufi "m""w""a" na wawili wakiwa wameshikilia silabi: "li""mu" 8. Endelea na 'Tunafanya': Waambie wanafunzi wabinye vidole na kupiga makofi kwa silabi pamoja na wewe. Elekeza kila mmoja aseme herufi ambazo zinaendana na kila silabi na omba wanaojitolea washikilie kadi herufi. Elekeza wanafunzi wote kuandika herufi ili kuunda neno (kwenye madaftari yao). 9. Malizia na 'Mnafanya': sema neno "mwalimu" na waeleze wanafunzi kila mmoja kwa kujitegemea, watenganishe sauti za herufi a silabi, watambue herufi ambazo zinaendana na sauti na silabi na kisha waandike neno kwenye madaftari yao.
KUPIMA	1. Wanafunzi wakishakuwa na uwezo wa kuficha maandishi peke yao, soma maneno mengine matatu kutoka kwenye orodha yako ya maneno. Waeleze wanafunzi waandike maneno kwenye madaftari yao.

Tathmini ya Ufundishaji: _____

Tathmini ya Ujifunzaji: _____

Maoni: _____

UFUATILIAJI

Baada ya kumaliza moduli hii, Mratibu Elimu wa Kata, Ofisa Elimu wa Wilaya na Mkaguzi Elimu wa Wilaya watafuatilia kuona namna unavyotumia mbinu za moduli hii darasani kwako. Wakati wa ufuatiliaji huu, ni vema ukawa na uwezo wa kuone sha mambo yafuatao:

a) Eleza mbinu za kuwasaidia wanafunzi kushikilia penseli na anza kuandika herufi moja moja
b) Eleza mchakato wa 'kuficha maandishi' na namna wanafunzi wanavyoweza kutumia ujuzi wao wa foniki kuandika maneno
c) Onesha namna ulivyotumia miongozo ya masomo kutoka katika moduli hii kwenye darasa lako.

MWISHO

WAAMBIE WALIMU:

"Walimu, tumefika mwisho wa moduli yetu, tumia dakika kumi kutafakari somo letu la leo. Jaza fomu kurekodi tathmini yako ya moduli. Baada ya kukamilisha chomoa ukurasa huo unipatie. Tafadhali uwe mkweli katika majibu yako kwa sababu yatasaidia kuboresha Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule hapo baadaye."

Kusanya fomu za tathmini zilizokamilishwa na walimu na uwe nazo wakati wa mkutano mwingine katika kundi la kata.

Wakati walimu wanaendelea kujaza fomu za tathmini, tafadhali tafakari kwa ujumla juu ya mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha siku hiyo na jaza visanduku vinavyofuata. Haya utaweza kuyajadili pamoja na Timu ya Wilaya ya Mafunzo Walimu Kazini na Waratibu wengine wa Mafunzo Walimu Kazini wa mkutano unaofuata katika kundi la kata.

MAFANIKIO YA JUMLA YA KIPINDI HIKI:	CHANGAMOTO ZA JUMLA ZA KIPINDI HIKI:

Shule: _____ **Wilaya:** _____ **Mkoa:**_____

Tafakuri za Moduli # _____ **Mada ya Moduli:** _____

Idadi ya walimu walioshiriki : _____ **Mwalimu Mkuu alishiriki : Ndiyo/Hapana**

MWISHO

MWISHO (DAKIKA 10)
Binafsi jaza fomu ifuatayo kuweka rekodi ya tathmini ya moduli ya leo. Baada ya kukamilisha, chomoa ukurasa huu na umpe Mratibu wako. Tafadhali uwe mkweli kwa vile mrejesho wako utasaidia kuboresha Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule hapo baadaye.

JEDWALI LA KUTATHMINI			
Alama 0: Sikubaliani kabisa na usemi huu	**Alama 1: Kwa kiasi Sikubaliani** na usemi huu	**Alama 2: Nakubaliana kwa kiasi** na usemi huu	**Alama 3: Nakubaliana Kabisa** na usemi huu

FOMU YA TATHMINI

Shule: _____ **Wilaya:** _____ **Mkoa:**_____

Tathmini ya Moduli: _____ **Mada ya Moduli:** _____

Idadi ya walimu walioshiriki: _____ **Mwalimu Mkuu alishiriki: Ndiyo/Hapana**

Mratibu alikuwepo kuwezesha: Ndiyo/Hapana

Soma semi zifuatazo kisha weka alama ya vema katika kisanduku husika kuonesha jibu lako:	**0**	**1**	**2**	**3**
1. Dhana kuu ya moduli ya leo ilikuwa inaeleweka.				
2. Moduli hii ina mikakati mingi mizuri na yenye manufaa ambayo nitaitumia darasani kwangu.				
3. Muda uliotumika kukamilisha moduli hii unafaa. Sikuhisi kwamba ni muda mrefu sana.				
4. Moduli hii iliibua mjadala wa kufurahisha na tafakuri ya hali ya juu sana.				
5. Violezo vya kipindi cha kusoma na kuandika vilisaidia sana. Natarajia vitakuwa rahisi kuvitumia ndani ya darasa langu.				
6. Zana tulizotengeneza leo zitakuwa za manufaa sana (kama inahusika).				
7. Mratibu amejiandaa kwa kipindi – amesoma vizuri moduli na ameandaa vifaa vyote vya kufundishia.				
8. Mratibu anasimamia vizuri majadiliano – anajua jinsi ya kuwafanya watu wajieleze na namna ya kupata majibu.				
9. Mratibu anajua namna ya kusimamia makundi – anahakikisha kuwa walimu wanatoa ushirikiano, wanashirikiana na wana hamasika.				
10. Mratibu anajua jinsi ya kuwahamasisha walimu – anafuatilia kujua waliokosa vipindi au kuchelewa na kutukumbusha kwanini Mafunzo ya Walimu Kazini ni muhimu kwetu.				